# JITEGEMEE HOLDINGS COMPANY LTD

# UFUPISHO

## ANDIKO LA MRADI WA UZALISHAJI WA KOKOTO CHAMWINO-DODOMA



**Juni 2024**

## 1.1 KUSUDIO LA UWEKEZAJI KATIKA MRADI WA KOKOTO

Jitegemee Holdings Company Ltd ni miongoni mwa kampuni zinazomilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya usimamizi wa Bodi ya Wakurugenzi. Dhima kuu ya kampuni hii ni kufanya shughuli za ushimbaji wa madini ya aina mbalimbali nchini pamoja na kufanya biashara zinazoendana na shughuli hizo. Aidha, hadi kufikia Mwezi Juni 2024 kampuni imekuwa ikishughulika na uchimbaji na usafirishaji wa Makaa ya Mawe Mkoani Ruvuma, Wilaya ya Mbinga Kijiji cha Ntunduwaro; mradi ambao kwasasa ni mradi mama wa kampuni. Sambamba na mradi huo, pia kampuni ipo katika mkakati wa kuendelea kuibua miradi mipya kulingana na vipaumbele vyake vya kiuwekezaji na rasilimali zilizopo.

Aidha, baada ya kujiimarisha katika mradi wa uchimbaji wa makaa ya mawe, kampuni ipo kwenye mkakati wa kupanua wigo wa mapato kuendelea kuanzisha miradi mingine ikiwemo mradi wa uzalishaji wa kokoto katika vitalu vya leseni Na. PML 1676 DOM na PML 1675 DOM zilizopo Kijiji cha Mjelo na Mnase katika Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma. Hivyo, kulingana na vipaumbele vya kiuwekezaji kampuni imeshafanya utafiti wa kijiolojia katika leseni hizo ili kubaini kiwango cha mishapo iliyopo na kuandaa andiko la mradi wa biashara.

Licha ya kufanya utafiti wa kubaini kiwango cha mishapo, taratibu za vipimo vya kimaabara pia zilifanyika ili kubaini ubora wa jiwe lililopo katika leseni hizo. Utaratibu huu ulihusisha uchukuaji wa sampuli za mawe na kupima katika maabara za madini za Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM) na Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ambapo matokeo ya vipimo yalionesha ubora mzuri wa jiwe unaokidhi matumizi ya ujenzi wa majengo na barabara kwa kiwango cha lami kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1 hapo chini.

**Jedwali Na. 1: Matokeo ya Vipimo vya Ubora wa Sampuli za Kokoto**

| **Test** | **Sample test results** | | **Acceptable Standards** | **Status/Remarks** |
|---|---|---|---|---|
| | **UDSM** | **DIT** | | |
| Aggregate Crushing Value | 18% | Not tested | ≤ 35% | Qualified Results |
| Los Angeles Abrasion test | 35.7% | 28% | ≤ 50% | Qualified Results |
| Aggregate Impact Value | 15% | 11.6% | ≤ 30% for Wearing course<br>≤ 35% for Bituminous macadam<br>≤ 40% for water bound macadam | Qualified Results |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | base course | |
| Soundness of sand by use of Sodium Sulphate | 0.67% | Not tested | ≤ 12%: for Sodium sulphate test<br>≤ 18% for Magnesium Sulphate | Qualified Results |
| Specific gravity and Water absorption of Coarse Aggregates | 2.6: Road construction<br>0.60: Road Surfacing | 2.6: Road Construction<br>0.70: Road Surfacing | 2.5 – 2.9: Road Construction<br>0.1 – 2.0: Road Surfacing | Qualified Results |
| Coating and Stripping of Aggregate Mixtures | > 95% | Not tested | ≥ 95% | Qualified Results |
| Ten Percent Fines Value-10% Fact | 198kN | 180kN | ≤ 400kN | Qualified Results |

Hivyo, baada ya tathmini ya kina kufanyika hususan kupitia matokeo ya kitafiti, kampuni inakusudia kuwekeza kwenye mradi wa uzalishaji wa kokoto katika kiwango cha mzalishaji wa kati mkoani Dodoma.

## 1.2 HALI YA UZALISHAJI NA SOKO LA KOKOTO DODOMA

Pamoja na kufanya utafiti wa kijiolojia, kampuni pia imefanya utafiti wa kimasoko ambapo utafiti umebaini kuwa kiasi kikubwa cha fursa ya soko la kokoto kinategemea zaidi miradi ya taasisi za Serikali; mashirika ya ujenzi na taasisi chache za watu binafsi hususan kampuni za kikandarasi. Taasisi hizo ni kama vile TANROADS, TARURA, National Housing Corporation na Watumishi Housing Corporation. Aidha, miradi mikubwa inayotegemewa ni ujenzi wa barabara kuu ya kuzunguka Jiji la Dodoma (Ring Road), sehemu ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa majengo ya Serikali, ujenzi wa uwanja wa ndege, ujenzi wa kiwanja cha michezo na ujenzi wa barabara kuelekea pembezoni mwa Jiji la Dodoma.

Hivyo, ni ukweli kwamba mahitaji ya kokoto kwa sasa ni makubwa ukizingatia kuwa ubora wa jiwe katika leseni zetu ni mkubwa na unafaa kwa matumizi yote ya ujenzi wa majengo na barabara. Hata hivyo, taarifa za ofisi ya Tume ya Madini ya Tanzania, zinaonesha kuwa, hali ya uzalishaji wa kokoto kwa sasa ni tani 470,000 hadi 590,000 kwa mwaka, ikiwa mahitaji yaliyopo ni tani 800,000 hadi 980,000 kwa mwaka. Uzalishaji huo unajumuisha wazalishaji wadogo, wakati na

wakubwa kama ilivyooneshwa kwenye Sehemu ya tatu ya andiko la mradi wa biashara.

## 1.3 TAARIFA ZA KIJIOLOJIA NA MAKADIRIO YA UZALISHAJI

Utafiti wa kijiolojia katika leseni Na. PML 1675 DOM na PML 1676 DOM unaonesha kuwepo kwa mishapo (reserve) ya jumla ya Mita za ujazo 574,522.66 sawa na tani 1,493,758.92 kwa kizio cha 2.6. Hivyo, kiasi hicho cha mishapo, kitakuwa na uwezo wa kuzalisha asilimia 73% ya kokoto safi ambazo ni sawa na tani 629,102.31 kwa kizio cha 1.5 katika kipindi chote cha mradi.

Kwa muktadha huo, kampuni ya JHCL inatarajia kuwekeza kwenye mitambo yenye uwezo kamili wa kuzalisha tani 50 kwa saa, sawa na tani 800 kwa siku yenye masaa 8 na awamu mbili za uzalishaji kwa siku (usiku na mchana). Uzalishaji halisi utakuwa ni 75% ya uwezo kamili wa mitambo hiyo, ambapo inakadiriwa jumla ya tani 15,000 zitazalishwa kila mwezi na tani 180,000 kwa mwaka kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 2 hapo chini. Hivyo, kwa kiwango hicho cha uzalishaji, inakadiriwa kuwa maisha ya mradi huu itakuwa ni miaka 3.5 kulingana na kiasi cha mishapo iliyopo kama ilivyoelezwa hapo juu.

## 1.4 MAKADIRIO YA FAIDA/HASARA YA MRADI

Katika hatua za utekelezaji wa mradi huu, kampuni inatarajia kuwekeza jumla ya Shilingi 4,460,000,000 kama mtaji hadi kukamilika kwake; gharama hizi zinahusisha ununuzi wa mitambo na vifaa, gari kwaajili ya shughuli za uendeshaji, lori kwa matumizi ya mgodini, pamoja na gharama za kianzio cha shughuli za uendeshaji kama ilivyoanishwa kwenye *Kiambata Na. II-IV na Sehemu ya Nne* katika andiko la mradi.

Katika Jedwali Na. 2 na 3 hapo chini, imeanishwa mpango wa makadirio ya uzalishaji na mauzo kwa kipindi cha miaka 5 kwa kuzingatia dhana za kiuchumi na kibiashara zilizoainishwa *Sehemu ya Tatu* ya andiko la Mradi wa Biashara.

**Jedwali Na. 2: Mpango wa Uzalishaji na Mauzo kwa Miaka 5**

| Details/Years | Monthly | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Production Under Full Capacity (Ton) | 20,000 | 240,000 | 240,000 | 240,000 | 240,000 | 240,000 |
| Actual Production in MT (75%) | **15,000** | 180,000 | 180,000 | 185,400.00 | 190,962.00 | 196,690.86 |
| Sales Rates on | | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Production | | **100%** | **100%** | **100%** | **100%** | **100%** |
| Sales (Tons) | | 180,000.00 | 180,000.00 | 185,400.00 | 190,962.00 | 196,690.86 |
| Sales Price/Ton | | 36,000 | 36,000 | 36,000 | 36,000 | 36,000 |
| **Revenues (TSh)** | | **6,480,000,000** | **6,480,000,000** | **6,674,400,000** | **6,874,632,000** | **7,080,870,960** |

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Faida/Hasara na Uchambuzi wa Kiuwekezaji**

| No. | Items | Year-1 | Year-2 | Year-3 | Year-4 | Year-5 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Net Profit | 693,279,476 | 617,314,625 | 672,402,638 | 729,525,012 | 788,742,476 |
| 2. | Retained Earnings | 693,279,476 | 1,310,594,101 | 1,982,996,739 | 2,712,521,751 | 3,501,264,227 |
| 3. | Net Total Assets | 5,103,279,476 | 5,720,594,101 | 6,392,996,739 | 7,122,521,751 | 7,911,264,227 |
| 4. | Net Cash Flow | 1,147,779,476 | 1,222,314,625 | 1,126,902,638 | 1,184,025,012 | 1,243,242,476 |
| 5. | ROE | 15.72% | 14.00% | 15.25% | 16.54% | 17.89% |
| 6. | ROCE | 19.41% | 15.42% | 15.03% | 14.63% | 14.24% |
| 7. | Liquidity Ratio | 1.21 | 1.37 | 1.52 | 1.68 | 1.84 |
| 8. | **Net Present Value: TZS 169,062,214.41**<br>**Internal Rate of Return: 10.18%**<br>**Discounted Payback Period: 4.9 Years** | | | | | |

## 1.5 UWEZEKANO WA UTEKELEZAJI WA MRADI

Mizania na muongozo wa kutambua uwezekano wa utekelezaji wa mradi huu imefanyika kwa kuzingatia vikokotoo mbalimbali ikiwemo *'Net Present Value (NPV), Payback Period (PBP) na Internal Rate of Return (IRR)'* sambamba na vipimo vya ustahimilivu wa mradi kibiashara kama vile *'Liquidity ratios, Return on Capital na Return on Capita Employed'.* Aidha, kupitia Jedwali Na. 3 hapo juu vipimo vikokotoo na vipimo hivyo vinaonesha uwezekano chanya unaokidhi vigezo vya kuanzisha mradi huu na kuwa utakuwa himilivu kibiashara kwa muda mrefu.

Hata hivyo, kulingana na kiasi cha mishapo iliyopo na idadi ya miaka ya maisha ya mradi, inashauriwa kampuni kufanya yafuatayo:-

i. Kuongeza idadi ya leseni za vitalu vya kokoto karibu na leseni zilizopo kwasasa.
ii. Kuwekeza kiwango kidogo cha mtaji kwa kila awamu ya utekelezaji wa mradi.
iii. Kuepuka kukodi mitambo na vifaa vya uzalishaji kwa wingi.

iv. Kuendelea kufuatilia mwenendo wa soko la kokoto na/au kuteka soko maalum hususan la miradi ya Serikali Mkoa wa Dodoma.